


Afisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Onesmo Ngao, akizungumzia kuhusu kuingizwa zaidi ya tani 3,500 za mbolea mkoani humo. (Na Mpigapicha Wetu)

# Bei elekezi ya mbolea itakavyoongeza mavuno ya chakula mkoani Ruvuma

*Na Albano Midelo*

MKOA wa Ruvuma umefanikiwa kushika nafasi ya kwanza katika uzalishaji wa mazao ya chakula nchini katika msimu wa kilimo 2018/2019.

Takwimu zinaonesha kuwa katika msimu wa mwaka 2019/2020 Mkoa wa Ruvuma ulilima hekta 268,008 zilizotoa mavuno ya tani 787,321 hii ni sawa na ongezeko la tani 50,628.

Mkuu wa Mkoa (RC) Ruvuma, Christina Mndeme anasema mafanikio hayo yametokana na uwepo wa nguvu kazi ya kutosha na utayari wa wananchi kushiriki katika shughuli za uzalishaji katika kilimo ambapo hadi sasa mkoa una chakula cha kutosha na ziada.

"Mkoa una jumla ya hekta 4,007,746 za ardhi zinazofaa kwa kilimo, katika kipindi cha Miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 Mkoa umeweza kuzalisha tani 8,547,816 za mazao," mkuu wa mkoa anasema.

Anataja mahitaji ya chakula katika Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka 2020 kuwa ni tani 469,172 ikilinganishwa na uzalishaji wa mazao ya chakula ni tani 1,346,220 na hivyo kuufanya mkoa kuwa na ziada ya chakula tani 877,048.

Anasema kuwa uzalishaji huo umechangiwa na matumizi ya zana bora za kilimo na matumizi ya pembejeo za kilimo kama mbolea na mbegu bora na kwamba matumizi ya mbolea yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka.

Takwimu zinaonesha kuwa toka mwaka 2015 hadi kufikia 2020 mbolea iliyotumika katika Mkoa wa Ruvuma ni jumla ya tani 167,758.5 ambapo anasema kiasi hicho cha mbolea kimepatikana kutokana na serikali kuandaa mazingira mazuri ya uingizaji wa mbolea nchini.

Wakulima wa Mkoa wa Ruvuma wakiwa katika maandalizi ya msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2020/2021 tayari serikali imetoa bei elekezi ya mbolea ya kupandia na kukuzia kwa wauzaji wa mbolea ya jumla na rejareja ili kuhakikisha mkulima ananunua mbolea kwa gharama nafuu.

Christian Mhando, Mkaguzi wa Mbolea Mamlaka ya Kudhibiti Mbolea Tanzania (TFRA), akizungumza baada ya kukagua kampuni saba za kuuza mbolea mkoani Ruvuma, anasema kuwa mkoa huo una mawakala wa kuuza mbolea zaidi ya 120,anatoa onyo kwa wafanyabiashara kuhakikisha wanauza mbolea kwa bei elekezi kwa mbolea zote za kupandia na kukuzia.

"Wafanyabiashara hao wahakikishe wanatoa risiti za mashine mara baada ya kuuza mbolea hizo kwa wananchi, pia wauze mbolea ambazo zimesajiriwa na TFRA na kuzingatia utunzaji bora wa mbolea kwa kuwauzia wakulima mbolea zenye ubora, na yeyote atakayekwenda kinyume na maelekezo hayo atachukuliwa hatua," Mhando anasema.

Mkaguzi huyo wa mbolea anawatahadhari wafanyabiashara kuacha tabia ya kuuza mifuko ya mbolea ambayo imefunguliwa ambapo anasema TFRA itachukua hatua Kali ikiwemo kuwanyang'anya leseni, kufunga biashara na kupelekwa mahakamani ili kufunguliwa mashitaka kwa mujibu wa sheria ya mbolea.

Hata hivyo, anasema kuwa imebainika baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wanakiuka bei elekezi ya mbolea kwa kuongeza bei na kwamba changamoto hiyo imekuwa inajitokeza zaidi ya kwa wafanyabiashara wadogo ambapo amezipongeza kampuni za uuzaji wa mbolea kwa kuzingatia bei elekezi na kwamba baadhi ya kampuni zimekuwa zinauza chini ya bei elekezi hivyo kuleta unafuu kwa wakulima.

Kwamba, kutokana na changamoto hizo kila mwaka wamekuwa wanakutana na wadau wa mbolea wakiwemo wawakilishi wa wakulima ,wafanyabiashara wa mbolea na kampuni za mbolea ambapo wanapanga bei kwa pamoja na kuridhiwa na waziri wa kilimo kisha kutangaza bei elekezi.

Amesisitiza kuwa, bei elekezi za mbolea za Tanzania zimekuwa rafiki kwa wakulima ukilinganisha na nchi nyingine hasa katika kipindi hiki cha janga la corona ambapo imebainika bei ya mbolea ya Tanzania ni ya chini zaidi hivyo kuleta unafuu kwa wakulima.

"Ukiangalia katika Mkoa wa Ruvuma katika msimu huu, mbolea ya kupandia bei yake haitazidi shilingi 50,000 kwa mfuko na mbolea ya kukuzia itakuwa kati ya shilingi 46,000 hadi 47,000 itategemea na mazingira ambayo mkulima yupo," amesema.

Anasema kuwa serikali ya awamu ya tano inaendelea kujitahidi kuhakikisha kuwa bei ya mbolea kwa mkulima inaendelea kupungua na kwamba awali mfuko mmoja wa mbolea ulifikia zaidi ya shilingi laki moja ambapo hivi sasa imeshuka hadi kufikia chini ya shilingi 50,000.

Anasisitiza kuwa mbolea ya Tanzania inauzwa kwa gharama nafuu hali inayosababisha wakati mwingine wafanyabiashara kutorosha mbolea hiyo kwenda kuuza katika nchi za jirani.

Mhando anabainisha zaidi kuwa, serikali ya awamu ya tano imeondoa tozo zaidi ya 114 ambazo ilikuwa zinaathiri wakulima, hali ambayo imesababisha bei ya mbolea kuendelea kupungua.

Afisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Onesmo Ngao anatoa rai kwa wakulima kuhakikisha wananunua mbolea yenye ubora na hasa katika kipindi hiki ambacho tayari serikali imetoa bei elekezi ya mbolea katika Mkoa wa Ruvuma na taifa kwa ujumla.

Ngao anataja mahitaji ya mbolea katika Mkoa wa Ruvuma kwa msimu ujao wa 2020/2021 kuwa ni tani 50,000, na kwamba serikali inaendelea kuhimiza kampuni za mbolea kuingiza mbolea ambapo hadi sasa mbolea ambayo imeingizwa katika Mkoa wa Ruvuma ni zaidi ya tani 3,500 na juhudi za kupeleka mbolea vijijini kwenye wakulima wengi zinaendelea.

**Mahitaji ya mbolea Mkoa wa Ruvuma msimu ujao wa 2020/2021 ni tani 50,000. Mkoa huo msimu huu mwaka 2019/2020 zililimwa hekta 268,008 za mazao mbalimbali, mavuno ilikuwa tani 787,321, sawa na ongezeko la tani 50,628 ...**

"Sisi kama watalaam wa kilimo Mkoa wa Ruvuma, tumekuwa tunahimiza wakulima kujiunga katika vikundi vya wakulima ili wafanyabiashara waweze kuwapelekea mbolea katika maeneo yao kwa gharama nafuu badala ya wao kuja mmoja mmoja mjini kununua mbolea," Ngao amesisitiza.

Akibainisha zaidi, anasema kuwa katika msimu huu kuna mbolea ya kutosha na kwamba bado mbolea inaendelea kuingia katika Mkoa wa Ruvuma ili kuhakikisha kuwa Mkoa wa Ruvuma unakuwa na shehena ya kutosha ya mbolea kulingana na mahitaji ya wakulima.

Ametoa rai kwa wakulima mkoani Ruvuma katika kipindi hiki cha uuzaji wa mazao, kuwa wanunue mbolea kwa ajili ya matumizi ya msimu ujao wa kilimo, ambapo hivi sasa maduka mengi yanauza mbolea kwa bei iliyo elekezi.

Katika msimu wa mwaka 2019/2020 Mkoa wa Ruvuma ulilima hekta 268,008 za mazao mbalimbali, zilizotoa mavuno ya tani 787,321, sawa na ongezeko la tani 50,628.

Scanned with CamScanner